



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA



Juni 15, 2022

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Tamko la THBUB wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee Duniani, 2022

Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) inaungana na wadau wote ulimwenguni kuadhimisha **Siku ya Kupinga Ukatili Dhidi ya Wazee**. Siku hii ilipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa Desemba 19, 2011 kuitia Azimio Na. 66/127. Lengo la kuwepo kwa siku hii ni kuhamasisha jamii ulimwenguni kote kuhusu dhulma dhidi ya wazee. Kauli mbiu ya maadhimisho kitaifa kwa mwaka huu ni: **“Tuhakikishe Wazee wanalindwa, wanasikilizwa na kuheshimiwa, tusikose kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi.”**

Tume inatambua na kupongeza jitihada zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kujali ustawi wa wazee nchini. Mionganini mwa jitihada hizo ni pamoja na: Kujenga na kuhudumia makazi maalum kwa ajili ya wazee; Matibabu bure kwa wazee na kuweka madirisha ya kuhudumia wazee katika hospitali na vituo vya afya; Mfuko wa TASAF kuendelea kufadhili miradi kwa wazee; Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kulipa pensheni jamii kwa wazee wote wenye umri zaidi ya miaka 70; na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuendelea kuhudumia wastaafuli.

Pamoja na jitihada hizi, wazee bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zinazovunja haki zao, zikiwemo: Umaskini wa kipato; Manyanyaso au unyanyapaa; Mauaji yatokanayo na imani za kishirikina; Kutoshirikishwa katika ngazi za maamuzi; na Ukosefu wa Sheria ya ulinzi wa haki ya Wazee.

Kutokana na changamoto hizo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatoa mapendekazo yafuatayo kwa Serikali, wadau na jamii kwa ujumla:

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Kitalu Na. 201, Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chragg.go.tz, zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz

- i) Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Wazee ya mwaka 2003.
- ii) Ofisi ya Rais TAMISEMI iandae Mwongozo wa kuendesha Mabaraza ya Wazee na itenye fungu la kuendesha Mabaraza hayo kuanzia ngazi za vijiji hadi taifa.
- iii) Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ikishirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI iweka utaratibu wa kuwatambua Wazee wenye umri zaidi ya miaka 60 na kuwapatia vitambulisho vya Bima ya Afya iliyoboreshwa (ICHF).
- iv) Serikali iharakishe utaratibu wa upatikanaji wa pesheni jamii kwa wazee wote Tanzania Bara kama inavyofanyika Zanzibar.
- v) Serikali, kwa kushirikiana na wadau itoe elimu kwa jamii kuhusu umuhimu na wajibu wa kuwatunza wazee na kuepuka kuwatelekeza.
- vi) Vyombo vya ulinzi na usalama viendeleze jithada katika kutokomeza mauaji na ukatili dhidi ya wazee.
- vii) Wazee na wananchi wote wajitokeze kuhesabiwa katika Sensa ya Watu na Makazi Agosti 23, 2022 kwa maendeleo ya nchi yetu.

THBUB inaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wote katika kuhakikisha kuwa haki za wazee zinalindwa, zinahifadhiwa na kukuzwa hapa nchini.

“Tuhakikishe Wazee wanalindwa, wanasilizwa na kuheshimiwa, tusikose kuhesabiwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi.”

Imetolewa na:



Mohamed Khamis Hamad
Makamu Mwenyekiti

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Juni 15, 2022

TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA

Kitalu Na. 339, Mtaa wa Nyerere – Kilimani, S.L.P 1049, DODOMA/ Kitalu Na. 201, Mbweni, S.L.P 285, ZANZIBAR

Simu: +255 734 047 775/734 119 978 (Makao Makuu); +255 (24) 2230494 (Zanzibar)

Barua Pepe: info@chragg.go.tz, zanzibar@chragg.go.tz; Tovuti: www.chragg.go.tz